TANGAZO LA SERIKALI NA. 850 la tarehe 17/11/2023

SHERIA YA USIMAMIZI NA TOZO YA USHURU
(SURA. 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MAWILI YA PROGRAMU YA KITAIFA YA UFUATILIAJI WA HUDUMA ZA AFYA KATIKA AFUA ZA KIFUA KIKUU NA UKOMA WA WIZARA YA AFYA YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Mawili ya Programu ya Ufuatiliaji wa Huduma za Afya katika Afua za Kifua Kikuu na Ukoma ya Mwaka 2023 na itaanza kutumika kuanzia tarehe 10 Oktoba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuimarishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na magari mawili yaliyoainishwa kwenye Jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na kwa niaba ya Wizara ya Afya kwa ajili ya programu ya ufuatiliaji wa huduma za afya katika afua za kifua kikuu na ukoma, kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika Ukomo tarehe 19 Aprili, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Namba ya Chasis | Idadi | Eneo la Ununuzi Ndani ya Nchi/ Nje ya Nchi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Toyota Fortuner | AHTKA3FS300624586 | 01 | Nje ya Nchi |
| 2. | Toyota Double Cabin Pickup | AHTFB8CD003875906 | 01 | Nje ya Nchi |

Dodoma,
9 Novemba, 2023.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*